



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA  
BARAZA LA WATAALAMU WA MAABARA**



Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)

## **TANGAZO**

### **KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA MITIHANI YA USAJILI**

Baraza la Wataalamu wa Maabara linachukua nafasi hii kuwajulisha Wataalamu wote wanaotarajia kufanya maombi ya mitihani ya usajili kwa ngazi za Astashahada (Certificate) na Stashada (Diploma) kuwa dirisha la maombi ya usajili limefunguliwa tarehe **11 Augusti 2022** na litafungwa tarehe **20 Septemba 2022 saa 9:30 alasiri**. Dirisha la maombi ya mitihani ngazi ya Shahada litafunguliwa hapo baadaye kwa taarifa.

Watahiniwa wote watatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo;

1. Wataalamu wenye usajili wa awali (PRP) ambao umekwisha muda au umebakiza miezi 2 na wale wa Marudio (Supplementary) ndio watatakiwa kufanya maombi ya mitihani.
2. Maombi ya kupata "Control number" kwa ajili ya malipo yatumwe kwa njia ya ujumbe mfupi (SMS) kwenda 0734005777 yakiwa na Majina kamili, Namba ya usajili wa awali (PRP), Kiasi kinacholipiwa, kituo unachopenda kufanyia mitihani na aina ya mitihani utakaofanya (First sit/Supplementary). Ikiwa ni supplementary lazima ainishe kama ni nadharia, vitendo au yote.
3. Baada ya dirisha kufungwa, orodha ya watahiniwa na vituo vyao vya mitihani vitawekwa kwenye tovuti ya Baraza ([www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)).
4. Vituo vya mitihani ni: KCMUCo-Kilimanjaro, Chuo cha Afya Amenye- Mbeya, CUHAS-Bugando Mwanza, UDOM-Dodoma, MUHAS-DSM na Chuo cha Afya St. Joseph-Tegeta DSM. Chuo cha Afya St. Joseph ni kwa ajili ya ngazi ya Stashahada tu ila kwa vituo vingine ni kwa mitihani ya ngazi zote.

**Angalizo:** 1. Maombi haya **HAYAFANYIKI** kwenye mfumo wa Baraza (HPRS) kwa sasa hivyo kwa msaada zaidi piga simu ya ofisi 0734005777.

2. **Maombi yatakayotumwa Baada ya tarehe 20 Septemba 2022 saa 9:30 Alasiri HAYATAFANYIWA KAZI**

Upatapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.

Imetolewa na



Msajili

Baraza la Wataalamu wa Maabara.

